

Public education  
Discover a world of opportunities

# KUSOMA: KUSOMEA NYUMBANI

## MAWAZO ZAIDI YA KUSOMA

### Kusoma pamoja

Wakati unaposoma na watoto wako:

- wahimize kusoma na wewe
- zungumzia kilichotokea kwenye hadithi na picha
- waonyeshe maneno muhimu katika hadithi na kuwelezea maneno hayo ili waweze kuyajua
- waombe wakuonyeshe maneno wanayoyajua

**Kucheza michezo ya kujifanyisha kama vile duka, shule, karakana, nyumba na mkaahawa husaidia watoto wajifunza juu ya maneno na vile kusoma hutumika katika maisha ya kila siku.**

- simama na uliza: *Unafikiri itatokezea nini? na Kwa nini unafikiria hivyo?* – kubali majibu yao hata kama siyo sawa
- wahimize kujiunga na maneno au misemo ya sauti mara kwa mara kupitia hadithi
- uliza swalikwa *nini* mfano: *Kwa nini unafikiri mwandishi ameweka hiki katika hadithi?*
- kujibu maswali yao hata kama wataingilia mtiririko wa hadithi – kumbuka uliuliza kutaka maoni yao!

**Soma vitu watoto wako wanavyovifurahia kweli ili waweze kujifunza kupenda kusoma!**

**Wakati watoto wenu wakifikia neno hawalijui, watie moyo kuangalia herufi ya neno na kujaribu sauti nje za sehemu zote au nusu ya neno – wape muda wa kufanya hivyo.**

Baada ya kumaliza kusoma na mtoto wako:

- wafanye warudie hadithi kwa maneno yao wenyewe kwako au kwa ndugu mwingine wa familia
- Uliza kuhusu matukio na wahusika, kwa mfano: *Ni mshirika mgani uliyompenda zaidi? na Tukio hilo lilifanyika wapi?*
- linganisha wahusika katika kitabu na watu unaowajua
- zungumzia kwa nini kitabu kiliandikwa na ujumbe katika hadithi
- waulize wamejifunza kitu gani kama kitabu kina mafunzo mbalimbali
- waonyeshe jina la mwandishi na kama wamefurahia kitabu, pendekeza kusoma kitabu kingine cha mwandishi huyo huyo.

**Vile unavyosoma hadithi kwa watoto wako inaweza kuleta tofauti kubwa kulingana na jinsi wanavyoifurahia. Fanya sauti za wanyama mbalimbali na kubadilisha sauti yako kutokana na wahusika mbalimbali.**



Department of  
Education

utapata zaidi  
Kijitabu cha ukweli cha kusomea nyumbani  
Kwenye elimu hapa: [education.wa.edu.au](http://education.wa.edu.au).